**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2026 (THE FINANCE BILL, 2026)

**DODOMA,**

**JUNI, 2026**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 **(The Finance Act, 2026)** pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili.**

2. ***Mheshimiwa Spika*****,** awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi** kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri ili kuuboresha.

3. ***Mheshimiwa Spika*****,** napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya Kamati. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waandishi wa Sheria na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao kuhusu Muswada huu.

4. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/27 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 11 Juni, 2026 na kupitishwa hapa Bungeni jana tarehe 23 Juni, 2026.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** **Muswada huu kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** unakusudia kurekebisha Sheria mbalimbali za kodi na zisizo za kodi kwa lengo kubadili viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali za kodi pamoja na kuboresha mazingira ya biashara, kuweka na kuboresha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali, ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususani katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, nishati na afya ili kuongeza tija na uzalishaji, kukuza ajira na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

6. ***Mheshimiwa Spika*****,** Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu ni zifuatazo:-

   (i) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;

(ii) Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442;
(iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
(iv) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
(v) Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;
(vi) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
(vii) Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;
(viii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
(ix) Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Sura ya 38;
(x) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113
(xi) Sheria ya Ukadiriaji Majengo Katika Serikali za Mitaa, Sura ya 289;
(xii) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
(xiii) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
(xiv) Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;
(xv) Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango, Sura ya 127;
(xvi) Sheria ya Reli, Sura ya 170;
(xvii) Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
(xviii) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168;
(xix) Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189;
(xx) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
(xxi) Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408;
(xxii) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
(xxiii) Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;
(xxiv) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148;
(xxv) Sheria ya Elimu na Mafunzo na Ufundi Stadi, Sura ya 82; na
(xxvi) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

7. ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kutoa maelezo kuhusu maudhui ya Muswada huu, napenda kutoa taarifa kwenye Bunge lako kwamba wakati wa majadiliano baina ya Serikali na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada huu yaliyofanyika kuanzia tarehe 14 hadi tarehe 24 Juni, 2026, tulikubaliana kufanya maboresho mbalimbali katika maeneo ya Muswada ikiwemo;

(a) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa wa asilimia 20 kwenye magari yenye umri wa miaka nane lakini hayazidi miaka kumi iliyopendekezwa kwenye Muswada hadi asilimia 18;

(b) Kupunguza ushuru wa bidhaa wa asilimia 40 uliopendekezwa kwenye Muswada kwa magari yenye umri wa zaidi ya miaka kumi lakini hayazidi miaka ishirini, hadi asilimia 35;

(c) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa magari yenye miaka inayozidi ishirini na kuendelea uliopendekezwa kwenye Muswada kutoka asilimia 50 asilimia 40;

(d) Kuondoa pendekezo la kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye thamani ya dau la michezo ya kubahatisha kama ilivyokuwa imependekezwa kwenye Ibara ya 9 ya Muswada;

(e) Kuweka masharti kuhusu msamaha katika Framework Agreements baina ya Serikali na kampuni za madini, ambapo tumekubaliana na Kamati kwamba, msamaha husika hautahusisha bidhaa za mafuta, utatolewa kwenye kipindi cha ujenzi wa mradi pekee na utamaliza muda wake pale tu kampuni husika zitakapoanza uzalishaji wa madini. Aidha, kampuni itakayotumia vibaya misamaha husika itachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kusitishiwa misamaha husika na kurejesha kodi yoyote waliyosamehewa;

(f) Kuondoa pendekezo la kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye pikipiki kama ilivyokuwa imependekezwa kwenye Ibara ya 11(g) ya Muswada;

(g) Kuondoa pendekezo la kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia moja (1) kwenye malipo yanayohusu mazao ya kilimo, wanyama hai, maziwa, Samaki, na mabondo kama ilivyokuwa imependekezwa kwenye Ibara ya 25 ya Muswada;

(h) Kuondoa pendekezo la kutoza kodi kwa utaratibu wa malipo ya mkupuo kwa asilimia moja (1) katika mapato yanayotokana na mazao ya kilimo kama ilivyokuwa imependekezwa kwenye Ibara ya 28 ya Muswada;

(i) kupunguza kiwango cha kodi kwa walipa kodi chini ya utaratibu wa makadirio kutoka kiwango cha asilimia 4.5 kinachopendekezwa kwenye Muswada hadi asilimia 4 kwa mapato yanayoanzia shilingi 11,000,001 hadi 200,000,000;

(j) Kuongeza wigo wa matumizi ya asilimia 5 inayotokana na mgawanyo wa mapato ya tozo ya maendeleo ya reli kutumika pia kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uongezaji thamani;

(k) kuondoa tozo ya shilingi kumi kwa sukari inayozalishwa nchini iliyopendekezwa kupitia Muswada huu na na badala yake kuweka tozo kwa sukari inayoagizwa nchini.

**MAUDHUI YA MUSWADA:**

8. ***Mheshimiwa Spika***, Muswada huu umegawanyika katika sehemu **Ishirini na Saba** kama ifuatavyo: -

9. ***Mheshimiwa Spika*, Sehemu ya Kwanza,** yenye Ibara ya 1 na 2 inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1, Julai, 2026 isipokuwa pale itakapobainishwa vinginevyo.

10. ***Mheshimiwa Spika,* Sehemu ya Pili** yenye Ibara za 3 hadi 5, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197** kama ifuatavyo:

    (a) Ibara ya 4 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 35(2) ili kupunguza kiwango cha ukomo wa mkopo wa muda mfupi (overdraft) kutoka asilimia 18 ya mapato halisi ya ndani ya mwaka wa fedha uliopita hadi asilimia 14. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; na

    (b) Kufuatia mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Serikali imeridhia kufuta Ibara ya 5 yenye mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha 69 ili kubainisha vigezo ambavyo Benki inaweza kuruhusu mikopo ya muda mfupi kwa Serikali endapo kutatokea matukio ya dharura na yasiyotabirika.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Tatu** yenye Ibara ya 6 na 7, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 13 cha **Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442** ili; Mosi, kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuainisha malipo yanayopaswa kufanyika kwa njia ya kielektroniki na Pili, kuweka sharti la uthibitisho wa malipo ya kidijitali kuwa rejea ya lazima itakayotumika kuidhinisha maombi ya uhamishaji wa mali kama vile ardhi, majengo na vyombo vya moto. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi na hivyo kuzuia vitendo vya uhalifu utakatishaji fedha, kupunguza gharama za kutunza, kusafirisha na kuchapisha fedha, pamoja na kurahisisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Nne** yenye Ibara za 8 hadi 11 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 9 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 126 kwa;

(i) kuondoa utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru kila baada ya miaka mitatu na badala yake, kuweka utaratibu wa kubadilisha viwango maalumu vya ushuru kila mwaka kwa kutumia kiwango cha mfumuko wa bei wa mwezi Machi kwa mwaka uliopita ikijumlishwa na asilimia 2. Lengo la marekebisho haya ni kuakisi thamani ya mapato ya Serikali na kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji;

(ii) kuongeza masharti kuhusu utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa watoa huduma wa kigeni kwa njia ya mtandao wasio na makazi ya biashara nchini na wanaouza moja kwa moja kwa mtumiaji wa mwisho ambao hawajasajiliwa au kutakiwa kuwasilisha ritani chini ya Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na misingi ya usawa ya utozaji kodi pamoja na kuhakikisha ushindani wa haki baina ya watoa huduma wa kawaida na wa mtandao;

(iii) kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini kutoka asilimia 15 hadi asilimia 18 kwa magari yenye umri wa miaka nane lakini hayazidi miaka kumi, na asilimia 35 kwa magari yenye umri wa zaidi ya miaka kumi lakini hayazidi miaka 20. Aidha, magari yenye miaka inayozidi 20 na kuendelea yatatozwa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 40. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kupunguza uingizaji wa magari husika ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha uchafuzi wa mazingira;

(b) Ibara ya 10 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 146B ili kuwezesha utoaji wa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa wawekezaji wa madini wenye Framework Agreements na Serikali baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Aidha, msamaha husika utatolewa kwenye hatua za ujenzi wa mradi na hautahusisha bidhaa za mafuta. Lengo la marekebisho haya ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika, kuhamasisha uwekezaji na kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati;

(c) Ibara ya 11 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Jedwali la Nne kwa:

(i) kurekebisha viwango maalum vya bidhaa mbalimbali zinazotozwa ushuru wa bidhaa kwa ongezeko la asilimia 8, ili kuakisi thamani ya viwango vya kodi kwa mwaka wa sasa na kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji;

(ii) kutoza kiwango cha asilimia 20 kwenye maua bandia, matawi ya bandia, matunda ya bandia pamoja na bidhaa zinazofanana na hizo zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Heading 67.02. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na matumizi ya bidhaa husika, kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali;

(iii) kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mashine za kukaushia rangi za kucha zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 8516.79.00. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza athari za kiafya zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya bidhaa husika ikiwemo ugonjwa wa saratani na kuongeza wigo wa kodi;

(iv) kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka asilimia 10 hadi asilimia 15 kwenye bidhaa za urembo zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa Headings 33.03; 33.04; 33.05 na 33.07. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali na kuwianisha viwango husika na viwango vinavyotozwa na baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(v) kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye viatu vya plastiki vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa HS Code 6402.99.00. Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha viatu vya plastiki na kuchochea uwekezaji ndani ya nchi; na

(vi) kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye magari yanayotambulika kwa HS Code 8703.21.90 yenye ukubwa wa injini (CC) usiozidi 1,000. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Tano** yenye Ibara ya 12 na 13 inapendekeza marekebisho katika Jedwali la **Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196** ili kuweka tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha;

(a) asilimia 30 ya thamani ya mzigo (FOB) au shilingi 200 kwa kila kilogramu moja kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye taka za

karatasi (waste paper) zinazotambulika kwa HS Code 4707.00.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea uongezaji wa thamani nchini na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi hiyo kwa wazalishaji wa karatasi na maboksi nchini;

(b) asilimia 10 ya thamani ya mzigo (FOB) au shilingi 200 kwa kila kilogramu kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye madini ya *Quartz* yanayotambulika kwa HS Heading 25.06 na *Feldspar* zinazotambulika kwa HS Code 2529.10.00. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha uwepo wa malighafi za kutosha kwa wazalishaji wa marumaru na vioo nchini; na

(c) shilingi 50 kwa kila kilo ya pumba za ngano (wheat bran) zinazotambulika kwa HS Code 2302.30.00; mashudu ya pamba (cotton cake) yanayotambulika kwa HS Code 2306.10.00; pumba za mpunga (rice bran) zinazotambulika kwa HS Code 2302.40.00; pumba za mahindi (maize bran) zinazotambulika kwa HS Code 2302.10.00; na mashudu ya alizeti (sunflower cake) yanayotambulika kwa HS Code 2306.30.00. Lengo hatua hii kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa bidhaa husika ambazo ni malighafi muhimu kwenye uzalishaji wa vyakula vya mifugo.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Sita** yenye Ibara ya 14 na 15 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 88 cha **Sheria ya Ushindani, Sura ya 285** ili kubainisha kuwa, mapato ya Baraza la Ushindani yanajumuisha asilimia 0.5 ya mapato ya mamlaka za udhibiti zilizoorodheshwa kwenye kifungu cha 88(1)(d) cha Sheria husika ikiwemo EWURA, LATRA, TCRA na TCAA. Hatua hii inalenga kutatua changamoto zilizopo ambapo sheria imebainisha vyanzo vya mapato na Taasisi zinazopaswa kuwasilisha sehemu ya mapato yake Baraza la Ushindani bila kuweka viwango husika.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Saba** yenye Ibara ya 16 na 17 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 34 cha **Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41** ili kuongeza kodi kwenye zawadi ya ushindi katika michezo ya kubahatisha hadi kufikia asilimia 15. Aidha,

maboresho yanafanyika kwenye mgawanyo ili kubainisha mgawanyo wa mapato yanayotozwa kwenye zawadi ya ushindi kwenye michezo ya kubashiri matokeo ambapo asilimia 7 ya mapato ya *land based casino* yanagawanywa kwa asilimia 70 kwenda Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na asilimia 30 itaelekezwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Aidha, asilimia 13 ya mapato ya *sport betting* yanagawanywa kwa asilimia 70 kwenda Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na asilimia 30 itaelekezwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Nane** yenye Ibara za 18 hadi 20 inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276** kama ifuatavyo;

    (a) Ibara ya 19 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 18A ili kuweka sharti la tozo ya maendeleo ya viwanda kutotozwa kwenye bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zinakidhi vigezo vya uasili (*Rules of Origins*). Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuruhusu vifungu na viwango vya utozaji kutumika kwa nchi mwanachama wa EAC pale itakapobainika kuwa, nchi husika imeweka vikwazo vya kibiashara kwa bidhaa zinazotoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vikijumuisha kutoza kodi, ada na tozo mbalimbali kwenye bidhaa hizo. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na matakwa ya Itifaki ya Uanzishwaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayoelekeza nchi wanachama kuzuia ubaguzi wa kikodi ili kuruhusu biashara huria na kuleta ushindani wa haki;

    (b) Ibara ya 20 inapendekeza kurekebisha Jedwali ili pamoja na mambo mengine:

        (i) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye madaftari (excercise books na notebooks) yanayoingizwa nchini yanayotambulika kwa HS Codes 4820.10.00 na 4820.20.00;

        (ii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye trela (trailers) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Codes 8716.31.90, 8716.39.90 na 8716.40.90;

(iii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye nyavu za kuvulia samaki zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 5608.11.00;

(iv) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye milango, madirisha, pamoja na fremu zake zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 7610.10.00;

(v) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye bidhaa za chuma (steel structure) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 7308.90.99; na

(vi) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye *aluminium structures* zinazotambulika kwa HS Code 7610.10.00.

Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Tisa** yenye Ibara za 21 hadi 31 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 22 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 10(3) ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ya kusamehe kodi ya mapato kwa kampuni za madini zenye Framework Agreements na Serikali baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Aidha, msamaha husika utatolewa kwa kipindi cha ujenzi wa mradi na hautahusisha kipindi cha uzalishaji;

(b) Ibara ya 23 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 33A ili kupunguza kiwango cha faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa (deemed retained earnings) kinachotozwa kodi ya zuio kutoka asilimia 30 hadi

asilimia 15. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuziondoa taasisi za fedha (financial institutions), bima, makampuni yaliyosajiliwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam pamoja na taasisi zenye mikataba ya utekelezaji na Serikali (Framework Agreements) katika utaratibu wa kutozwa kodi hiyo;

(c) Ibara ya 24 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 44 kwa kuondoa kodi iliyolipwa awali kwenye uhamisho wa mali mtaji kwa watu wenye uhusiano. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa katika mfumo wa utozaji kodi;

(d) Kufuta Ibara ya 25 iliyokuwa inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 109A ili kuweka masharti ya kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia moja (1) kwenye malipo yanayohusisha mazao ya kilimo, wanyama hai, maziwa ambayo hayajachakatwa, samaki ambao hawajachakatwa na mabondo;

(e) Ibara ya 26 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 116 ili kuongeza kiwango cha kodi ya mapato kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni kutoka asilimia 2 hadi asilimia 3. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali;

(f) Ibara ya 27 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 116A ili kuongeza wigo wa mapato yanayotokana na mazao ya misitu kwa kujumuisha mazao ya *natural varnish, latex, resin, sap* na *gums* yanayopaswa kutozwa kodi kwa utaratibu wa malipo ya mkupuo. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa kodi na kuendana na misingi ya usawa wa utozaji kodi;

(g) Kufuta Ibara ya 28 iliyokuwa inapendekeza kutoza kodi kwa utaratibu wa malipo ya mkupuo kwa asilimia moja (1) katika mapato yanayotokana na mazao ya kilimo;

(h) Ibara ya 29 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kuondoa sharti la kuwasilisha ritani kwa mtu aliyelipa kodi kwa mkupuo mmoja kwa mujibu wa kifungu cha 116A cha Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za utekelezaji wa wajibu wa ulipaji kodi;

(i) Kufuta Ibara ya 30 iliyokuwa inapendekeza kutambua masharti ya msamaha wa kodi ya mapato yaliyopo kwenye Framework Agreements baina ya Serikali na wawekezaji wa madini;

(j) Ibara ya 31 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza ili;

(i) kuongeza kima cha juu cha mauzo yanayotozwa kodi kwa utaratibu wa makadirio kutoka shilingi 100,000,000 hadi shilingi 200,000,000;

(ii) kuweka sharti la kuruhusu mlipakodi mwenye mauzo ya chini ya shilingi 200,000,000 kuandaa vitabu vya hesabu pale atakapoona inafaa kwa lengo la kutumia utaratibu wa kujikadiria kodi. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha kima husika na kima cha usajili wa kodi ya ongezeko la thamani pamoja na kuboresha mfumo wa kodi;

(iii) kuweka msamaha wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kupata Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (Taxpayer Identification Number -TIN). Msamaha huo ni kwa ajili ya wafanyabiashara waliopo chini ya utaratibu wa makadirio (presumptive regime) pekee. Hatua hii inatofautiana na utaratibu wa sasa ambapo mfanyabiashara anaposajiliwa anafanyiwa tathmini ya mapato anayotarajia kuyakusanya na kupaswa kulipa kodi husika ndani ya miezi sita. Aidha, baada ya kipindi cha muda wa mpito, wafanyabiashara husika watapaswa kuanza kulipa kodi kwa mujibu wa sheria. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wafanyabiashara wapya kupata muda

wa kutosha wa kujiandaa na mahitaji ya msingi, kuondoa usumbufu wakati wa kuanza biashara pamoja na kuhakikisha kuwa makadirio ya kodi yanazingatia uhalisia wa mapato yanayopatikana kutoka kwenye shughuli za biashara; na

(iv) kuongeza kiwango cha kodi kwa walipa kodi chini ya utaratibu wa makadirio kwenye mauzo yanayozidi shilingi 11,000,000 lakini yasiyozidi shilingi 200,000,000 kwa mwaka na kutoka kiwango cha utozaji wa asilimia 3.5 hadi asilimia 4.0. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na misingi ya usawa ya utozaji kwa kuhakikisha kodi husika inalipwa kwa kuzingatia uwiano wa mapato halisi yanayopatikana kwa walipa kodi wenye mapato sawa na wale wanaotofautiana.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi** yenye Ibara za 32 na 33 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 19 cha **Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025** ili kujumuisha vichwa vya trela (road tractors for semi-trailers) vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi vinavyotambulika kwa HS Codes 8701.21.90, 8701.22.90, 8701.23.90, 8701.24.90 na 8701.29.90 kwenye orodha ya bidhaa zisizostahili msamaha wa kodi (negative list). Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani, ajira na mapato ya Serikali.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Moja** yenye Ibara za 34 na 35 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 36 cha **Sheria ya Ardhi, Sura ya 113** ili kuweka mgawanyo wa asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi (land rent) yanayorejeshwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo: asilimia 10 kupelekwa Wizara yenye dhamana na masuala ya Ardhi na asilimia 10 kupelekwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika upimaji wa ardhi na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Mbili** yenye Ibara ya 36 hadi 51 kama ilivyorekebishwa zinapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ukadiriaji Majengo Katika Serikali za Mitaa, Sura ya 289** ili kuhamisha jukumu la

ukusanyaji wa kodi ya majengo kutoka TRA Kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, ukusanyaji wa kodi hii utaendelea kufanyika kupitia ununuzi wa umeme kwa LUKU au kwa utaratibu mwingine utakaobainishwa na mamlaka ya ukusanyaji kwa nyumba zisizo na umeme wa TANESCO

21. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Tatu** yenye Ibara ya 52 hadi 57 zinapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290** kama ifuatavyo;

    (a) kurekebisha vifungu vya 6 na 7 ili kupunguza kiwango cha mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka asilimia 20 hadi asilimia 10 kutokana na asilimia 10 ya mapato husika kuhamishiwa Wizara ya Ardhi;

    (b) kurekebisha Kifungu cha 34 ili kuipa Mamlaka za Serikali za Mitaa wajibu kwenye ukusanyaji wa ada mbalimbali za mabango na matangazo na pia kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ya kutangaza ada za matangazo, usimamizi na mgawanyo wa ada na kodi ya majengo chini ya Sheria hii; na

    (c) kurekebisha Kifungu cha 41 ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 15 ya mapato yao ya ndani badala ya asilimia 10 iliyopo sasa kwa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, kati ya asilimia 15 itakayotengwa, asilimia 10 itaelekezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa uwiano kama ilivyokuwa awali. Aidha, asilimia tano (5) itatumika kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi na maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasiriamali kwa mamlaka za Serikali za mtaa. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Nne** yenye Ibara ya 58 na 59 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 149A katika **Sheria ya Madini, Sura ya 123** ili kuweka masharti yanayoiwezesha

Wizara ya Madini kuanzisha mfuko wa utafiti wa madini (Geoscientific survey) nchini na kubakiza asilimia 10 ya mapato yatokanayo na sekta husika kwa ajili ya kugharamia tafiti hizo. Aidha, fedha hizo zitaingizwa kwenye akaunti maalumu itakayofunguliwa Benki Kuu, na matumizi yake kufanyika baada ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utafiti na uwekezaji katika sekta ya madini nchini.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Tano** yenye Ibara ya 60 na 61 inapendekeza marekebisho katika Jedwali la Kwanza la **Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124** ili kuongeza kiwango cha ada ya usajili wa pikipiki kutoka shilingi 95,000 hadi shilingi 150,000. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali bila kuathiri biashara ya usafirishaji kwa kutumia pikipiki.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Sita** yenye Ibara ya 62 na 63 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 6 cha **Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango, Sura ya 127** ili kuweka utaratibu kwa miradi ya maendeleo ya Kitaifa kutathminiwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo vigezo vya kiufundi, kifedha na kiuchumi kabla ya kuingizwa katika bajeti ya Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya Serikali.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Saba** yenye Ibara ya 64 na 65 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 72 cha **Sheria ya Reli, Sura ya 170** kwa;

(a) kusamehe tozo ya maendeleo ya reli kwenye mipira ya kinga yenye namba za utambuzi HS Code 4014.10.00. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uingizaji wa mipira hiyo nchini kwa kuwa inatumika kama vifaa tiba; na

(b) kuweka mgawanyo wa mapato ya tozo ya maendeleo ya reli kama ifuatavyo; asilimia 70 itawasilishwa moja kwa moja katika Mfuko wa Reli, asilimia 25 itawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na asilimia 5 itawasilishwa katika akaunti maalumu iliyopo Benki Kuu kwa ajili

ya ujenzi wa miundombinu saidizi katika maeneo maalumu ya kiuchumi au maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya nje na miundombinu kwa ajili ya uongezaji thamani.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Nane** yenye Ibara ya 66 hadi 68 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 67 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 ili kuweka mgawanyo wa mapato yanayokusanywa kama tozo ya barabara kama ifuatavyo; asilimia 70 itawasilishwa moja kwa moja katika Mfuko wa Barabara, asilimia 25 itawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na asilimia 5 itawasilishwa katika akaunti maalumu iliyopo Benki Kuu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu saidizi katika Maeneo Maalumu ya Kiuchumi au Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya Nchi. Vilevile, kuweka mgawanyo wa mapato yatokanayo na ushuru wa barabara na mafuta kwenye petroli na dizeli kwa TARURA, Mfuko wa Maji, Mfuko wa UKIMWI, Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uwezo wa kifedha ili kukidhi malengo ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Barabara pamoja na kuiwezesha Serikali kugharamia mahitaji yake ya lazima; na

(b) Ibara ya 68 iliyokuwa inapendekeza kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ya kusamehe tozo ya barabara kwenye kampuni za madini zenye Framework Agreements na Serikali imefutwa ili kulinda mapato ya Serikali yanayotokana na tozo kwenye bidhaa za mafuta.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Kumi na Tisa** yenye Ibara za 69 na 70 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 cha **Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168** ili kuruhusu gari au trela iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za usajili za Tanzania Zanzibar kutumika Tanzania Bara likiwa na namba za usajili za Tanzania Zanzibar, pale ambapo kodi zote kwenye gari au trela husika zimelipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ndani ya Tanzania-Bara. Aidha, masharti haya hayatatumika kwa gari au trela

lililohamishwa kwa matumizi ya muda mfupi (tranfer for temporary use) wa miezi 3 na kwamba utekelezaji wa masharti haya utaanza tarehe 1 Januari, 2027. Lengo la marekebisho haya ni kutatua changamoto zilizopo kwenye matumizi ya vyombo hivyo baina ya pande mbili za Muungano pasipo kuathiri mapato ya Serikali.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Ishirini** yenye Ibara za 71 hadi 74 inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 72 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2 ili kujumuisha hati za ubadilishanaji wa mali zinazohamishika kwenye wigo wa utozaji wa ushuru wa stempu katika fasili ya msamiati wa mkataba wa ukodishaji. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa msamiati huo kama ulivyotumika katika masharti ya sheria;

(b) Ibara ya 73 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 65 ili kubadili gharama ya kurejesha stempu ambazo hazijatumika kutoka senti kumi kwa kila shilingi au sehemu ya shilingi kuwa asilimia 10 ya thamani ya stempu. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha ukokotoaji wa marejesho, kuboresha ufanisi wa kiutawala, na kuongeza uwazi na uthabiti katika kushughulikia marejesho ya stempu ambazo hazijatumika au zilizoharibika; na

(c) Ibara ya 74 inapendekeza kurekebisha Jedwali ili;

(i) kuongeza kima cha thamani cha utozaji wa ushuru wa stempu kwenye Hati ya Mauzo ya mali kwa njia ya dhamana kutoka shilingi 1,000 hadi shilingi 10,000;

(ii) kuongeza kima cha juu cha ukomo wa utozaji wa ushuru wa stempu kwenye Hati ya Mauzo kwa njia ya dhamana kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 100,000;

(iii) kubadili wigo wa thamani ya mtaji kwenye Hati za Ubia pamoja na viwango vya ushuru wa stempu kwenye hati husika kwa kutoza kiwango cha shilingi 5,000 kwa Hati zenye thamani ya mitaji isiyozidi shilingi 1,000,000 na kiwango cha shilingi 10,000 kwa hati zinaozidi thamani ya mitaji ya shilingi 1,000,000;

(iv) kuongeza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye hundi kutoka shilingi 500 hadi shilingi 700;

(v) kuongeza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye Hati za Kusitisha Mikataba ya Ukodishaji kutoka shilingi 1000 hadi shilingi 2000;

(vi) Kutoza ushuru wa stempu kwa kiwango cha shilingi 5000 kwenye hati za ubadilishanaji wa mali;

(vii) Kutoza ushuru wa stempu kwa kiwango cha asilimia 0.5 kwenye hati ya uhamishaji wa ardhi ya matumizi ya kilimo.

Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa kodi pamoja na kulinda thamani ya fedha; kulinda thamani halisi ya mapato na kuakisi mwenendo wa mfumuko wa bei pamoja na ongezeko la kiasi cha miamala rasmi ya kifedha.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Ishirini na Moja** yenye Ibara ya 75 hadi 84 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 76 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 8A ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ya kubainisha mikataba ya msingi (Framework Agreements) kwa madhumuni ya kikodi;

(b) Ibara ya 77 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 22 ili kutoa muda sawa kwa mtu ambaye anawajibika kulipa kodi kutokana na ajira kusajiliwa kwa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kwa watu wote wanaowajibika kulipa kodi;

(c) Ibara ya 78 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 54 ili kuweka utaratibu wa kuwasilisha taarifa za wakandarasi kwa njia ya kielektroniki na kuhifadhi taarifa zinazotolewa na watu wengine. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwazi na kuimarisha uhiari wa kutii sheria za kodi;

(d) Ibara ya 79 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 62 ili kufanya rejea sahihi ya kifungu kilichokusudiwa kurejewa katika Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408 kuwa ni kifungu cha 16(1) badala ya kifungu cha 17(2)(a);

(e) Ibara ya 80 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 67 ili kuondoa sharti la ulipaji wa kodi ya pango. Lengo la marekebisho haya ni kukidhi urejeshaji wa mamlaka ya ukusanyaji wa kodi ya pango kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ukadiriaji Majengo Katika Serikali za Mitaa, Sura ya 289;

(f) Ibara ya 81 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 73 ili kumpa Kamishna Mkuu mamlaka ya kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara au kwa makubaliano ya moja kwa moja bidhaa zilizotaifishwa zinazoweza kuharibika haraka. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka kupotea kwa thamani ya bidhaa hizo na kulinda mapato ya Serikali;

(g) Ibara ya 82 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90 ili adhabu za kutokuzingatia upangaji wa bei za uhamisho zihesabiwe kwa kuzingatia thamani kamili ya marekebisho ya bei elekezi yaliyofanyika. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata katika utekelezaji wa Sheria na kuhakikisha usawa katika utoaji wa adhabu kwa walipakodi;

(h) Ibara ya 82 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90 ili adhabu za kutokuzingatia upangaji wa bei za uhamisho zihesabiwe kwa kuzingatia thamani kamili ya marekebisho ya bei elekezi yaliyofanyika. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata katika utekelezaji wa Sheria na kuhakikisha usawa katika utoaji wa adhabu kwa walipakodi;

(i) Kuongeza Ibara mpya ya 83 inayopendekeza kuongeza kifungu kipya cha 94A ili kuweka adhabu kwa kampuni zenye mikataba ya msingi na serikali kwa kutumia msamaha uliotolewa tofauti na yaliyokuwa madhumuni, kuhamisha bidhaa zilizosamehewa bila idhini ya Kamishna, na kutumia udanganyifu ili kupata/kunufaika na msamaha. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha kosa na adhabu na kulinda mapato ya Serikali;

(j) Ibara ya 83 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 95 ili kubainisha kosa sahihi linalokusudiwa katika Sheria; na

(k) Ibara ya 84 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza ili;

  (i) kuondoa Kodi ya Majengo katika orodha ya kodi zinazosimamiwa chini ya Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mgongano wa kisheria kati ya sheria za kodi na sheria za Serikali za Mitaa; na

  (ii) kulitambua tamko la Kodi ya Ongezeko la Thamani iliyozuiliwa kama taarifa ya kodi kwa madhumuni ya masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uhiari wa kuzingatia sheria za kodi.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Ishirini na Mbili** yenye Ibara za 85 hadi 87 inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408** ili pamoja na mambo mengine kuweka muda wa siku 90 kwa ajili ya kutatua mgogoro nje ya mahakama. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwepo wa muda wa kutosha wa kutafuta suluhu ya migogoro ya kodi kwa njia ya maridhiano.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Ishirini na Tatu** yenye Ibara za 88 na 89 inapendekeza marekebisho katika Jedwali la Kwanza la **Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399** ili kujumuisha Sheria ya Kudhibiti Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276 na Sheria ya Kodi ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya

Nchi, Sura ya 196 katika orodha ya sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, marekebisho yanaondoa Sheria ya Ukadiriaji Majengo ya Serikali za Mitaa, Sura ya 289 kuwa miongoni mwa Sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Ishirini na Nne** yenye Ibara za 90 hadi 91 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 25 cha **Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161** ili kuongeza kiasi cha shilingi ishirini kinachotozwa katika kila sigara elfu moja na shilingi ishirini inayotozwa katika kila kilo moja ya sukari inayoagizwa kutoka nje ya nchi kuwa chanzo cha mapato ya Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Lengo la marekebisho haya ni kugharamia huduma ya bima ya afya kwa watu wanaostahili kugharamiwa na Mfuko huo.

33. ***Mheshimiwa Spika***, **Sehemu ya Ishirini na Tano** yenye Ibara za 92 hadi 100 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 93 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 ili ili kubainisha viwango vya kodi ya zuio vinavyotumika kwa usambazaji wa bidhaa na utoaji wa huduma, pamoja na kuweka utaratibu wa kugawanya thamani ya miamala inayojumuisha bidhaa na huduma kwa wakati mmoja. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kuhakikisha kuwa kodi inayozuiliwa inakokotolewa na kukusanywa kwa usahihi na kwa njia iliyo wazi kwa wadau wote;

(b) Ibara ya 94 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 6 ili kutambua msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani bidhaa na huduma za kampuni za madini zenye Framework Agreements na Serikali na zilizoidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Aidha, msamaha husika utafikia tamati baada ya kuanza kwa uzalishaji na utahusisha kipindi cha ujenzi wa mradi pekee.. Lengo la marekebisho haya ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika na kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati;

(c) Ibara ya 95 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11 ili kufuta ahirisho la malipo ya kodi ya Ongezeko la thamani kwa bidhaa za mtaji zinazoingizwa nchini. Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa ili kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha mamlaka pale atakapoona inafaa kuanisha masharti ya kunufaika na ahirisho la kodi ya Ongezeko la thamani (VAT deferment) kwenye bidhaa za mtaji;

(d) Ibara ya 96 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 51 ili kuweka masharti yanayokusudia kupanua wigo wa usimamizi na utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma za kielektroniki zinazotolewa kupitia majukwaa ya kidijitali yanayosimamiwa na waendeshaji wa majukwaa hayo au wapatanishi mtandaoni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa aina za huduma za kimtandao au zinazotolewa kwa njia ya mawasiliano zinazopaswa kutozwa kodi;

(e) Ibara ya 97 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 71 ili kuweka jukumu kwa wakala wa kodi ya zuio kuwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kodi ya ongezeko la thamani iliyozuiliwa na kuwasilisha taarifa kuhusu kodi hiyo ndani ya siku kumi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwajibikaji wa mawakala wa kodi ya zuio na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati kwa ajili ya usimamizi wa kodi;

(f) Kufuatia pendekezo la Kamati, Ibara ya 98 inayohusu kuweka sharti la marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kulipwa ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi ya marejesho hayo imefutwa ili kulinda mapato ya Serikali;

(g) Ibara ya 100 inapendekeza kurekebisha Jedwali kwa;

  (i) kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye chakula cha mbwa na paka kinachotambulika kwa HS Heading 23.09.10.00 kinachozalishwa na kinachoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza

misamaha isiyo na tija ili kulinda mapato ya Serikali pamoja na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi;

(ii) kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyavu za kuvulia samaki zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 5608.11.00 na kuweka msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyuzi za *Polyester* zinazotambulika kwa HS Code 5402.20.00. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuvutia uwekezaji nchini;

(iii) kujumuisha vifungashio vya maziwa vinavyotambulika kwa HS Code 3920.20.90 vinavyozalishwa nchini na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Lengo la marekebisho haya ni kutoa unafuu kwenye sekta ya maziwa nchini na kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushindana kwenye masoko ya kikanda na kimataifa;

(iv) kujumuisha karatasi zinazotumika kutengeneza hati za kupandia ndege kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Lengo la marekebisho haya ni kutekeleza matakwa ya Mikataba ya Makubaliano ya Usafiri wa Anga ambayo Tanzania imeridhia, yanayoitaka Serikali kusamehe kodi kwenye hati husika kama ilivyobainishwa kwenye miongozo ya usafiri wa anga ya kimataifa;

(v) kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia Julai 1, 2026 mpaka Juni 30, 2027. Lengo la marekebisho haya ni kuweka unafuu wa bei ya mafuta ya kula nchini;

(vi) kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye turbojets, turbo-propellers na gas turbines nyinginezo zinazotambulika kwa HS Heading 84.11 pamoja na matairi ya ndege yanayotambulika kwa HS Code 4011.30.00. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuchochea uwekezaji kwenye sekta ya anga nchini;

(vii) kuweka masharti ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mita janja za mitungi gesi ya kupikia zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 9028.10.00 msamaha husika utatolewa kwa wasambazaji wa gesi ya kupikia pekee. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea matumizi ya nishati safi;

(viii) kuweka masharti ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vitakavyotumika katika vituo vya kuchaji magari yanayotumia umeme vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa HS Code 8504.40.00 na mtoa huduma aliyesajiliwa. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha matumizi ya nishati safi na kulinda mazingira

(ix) kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nguo na mavazi yanayozalishwa kwa kutumia pamba inayozalishwa ndani ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuchechemua ukuaji wa viwanda vinavyotumia malighafi ya pamba inayozalishwa nchini; na

(x) kufuta pendekezo la kuweka masharti ya kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vitakavyotumika katika vituo vya kuchaji magari yanayotumia umeme vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa HS Code 8504.40.00. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha matumizi ya nishati safi na kulinda mazingira.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Ishirini na Sita** yenye Ibara ya 101 na 102 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 19 cha **Sheria ya Elimu na**

**Mafunzo na Ufundi Stadi, Sura ya 82** ili ili kuweka bayana wigo wa msamaha kwa taasisi za Serikali zisizopaswa kulipa Tozo ya Maendeleo ya Ufundi Stadi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** **Sehemu ya Thelasini** yenye Ibara ya 103 na 104 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 8 cha **Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283** kinachohusu mgawanyo wa mapato yanayopaswa Kwenda TAWA na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ili kubainisha kwamba ada zinazolipwa kwenye utalii wa picha katika maeneo ya wazi (fees payable for non-consumptive tourism in open areas) ndio moja wapo ya ada zitakazogawanywa badala ya ada ya pango (concession fees). Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha mapato yanayokusanywa na TRA kutokana na upigaji picha wa kitalii kuweza kurejeshwa katika vijiji husika ambavyo ardhi yao inatumika kwa ajili ya shughuli hizo za upigaji picha wa kitalii.

36. ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya hatua nyingine za mapato zilizopo katika Hotuba ya Bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada huu, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali (Government Notices) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

**HITIMISHO:**

***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji **kisheria** wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2026/27. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

***KMO***

***WF***